ST. AUGUSTINE SEC. SCHOOL

P. O. BOX 31644, TAGASTE- DAR ES SALAAM

VIFUNGU MUHIMU VYA SHERIA NA KANUNI ZA KILA SIKU SHULENI

Shule ya Sekondari ya Mt. Augustino -Tagaste ni ya Kanisa Katoliki inayomilikiwa na Shirika la Mt. Augustino- Tanzania (OSA). Shule inaendeshwa kwa kufuata taratibu zote za Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi (Sheria ya Elimu Na. 25 ya 1978 na marekebisho yake ya Na. 10 ya Mwaka 1995). Lengo la kuanzishwa kwa shule hii ni kutoa elimu bora na kumjenga mwanafunzi katika maadili na mwenendo mwema.

Zifuatazo ni sheria na kanuni za kila siku hapa shuleni, zenye lengo la kuleta amani, umoja, mshikamano na furaha miongoni mwa wanafunzi, na timu nzima ya uongozi wa shule. Baadhi ya Sheria na Kanuni hizi zinasisitiza na kufafanua baadhi ya Sheria za Shule zilizotolewa kwa wazazi/walezi siku walipochukua fomu za kuchaguliwa kwa watoto kujiunga na shule yetu.

1) Kwa vile shule ni mahali pa kusoma inatakiwa pawe na hali ya ukimya daima, hasa darasani, kwenye maktaba, kwenye maabara, kwenye mabweni, n.k. Ni marufuku kupoteza muda wa masoma au wa kujifunza kwa kupiga kelele, kusoma na kuandika barua, kuangalia picha zisizo za kielimu, kuwa na madaftari ya nyimbo na *music stars* na magazeti na albums za aina yoyote, au vitabu vinavyohusu mapenzi. Mambo haya huchafua akili ya mwanafunzi, hupoteza muda wake, huharibu maadili yake na hivyo kupelekea kushindwa kutimiza malengo yaliyomleta hapa shuleni (**ufafanuzi Sheria ya Shule no. 10**).

2) Muda wa kusoma na kujisomea uliopangwa na Uongozi wa Shule unatosha. Ni marufuku kabisa kwa wanafunzi kuamka, au kuamshana kwa ajili ya kusoma. Mwanafunzi atatumia vizuri muda uliopangwa na si vinginevyo.

3) Shule itajitahidi kutoa chakula kinachofaa na kinacholingana na kiasi cha ada. Watoto watakula vyakula vifuatavyo: muda wa asubuhi watapata uji wa mahindi, uji wa soya, chai kwa skonzi na mikate. Muda wa mchana na jioni watakula:- wali maharage, mboga za majani, na matunda; wali nyama, mboga za majani na matunda; ugali maharage, mboga za majani na matunda. Zipo siku wanafunzi watakula kande. Chakula hiki kitaandaliwa kwa mchanganyiko maalumu na kutolewa katika ratiba ya siku husika kwa mpangilio maalumu. **Wazazi/walezi wanaombwa wasimlete mtoto hapa shuleni, ikiwa mtoto hawezi kuvumiIia kula vyakula vilivyotajwa hapo juu**. **Pia:**

   a) Hairuhusiwi kabisa kwa mwanafunzi kuleta chakula cha aina yoyote arudipo shuleni toka likizo, au arejeapo shuleni baada ya kupata kibali cha kutoka nje ya shule kwa sababu maalumu (**angalia Sheria za Shule no. 08 na 20**).

   b) Vile vile haturuhusu mwanafunzi kutumiwa kwa njia ya Posta au kuletewa vifurishi vyenye chakula toka kwa wazazi, ndugu na marafiki. Hii ni pamoja na nyakati za sikukuu na hata sikukuu ya kuzaliwa mtoto (birthday). Ikifahamika wazazi/walezi watamchukua mtoto wao ili wamlishe chakula wanachotaka na kwa muda wanaotaka, ila shule ataikosa (**angalia Sheria za Shule no. 08 na 20**).

   c) Ni marufuku kwa mwanafunzi kununua aina yoyote ya chakula nje ya shule kama matunda, maandazi, n.k. Hii ni kwa ajili ya nidhamu ya chakula na usalama wa afya yake (**angalia Sheria za Shule no. 08 na 20**).

   d) Hairuhusiwi kuchukua chakula nje ya Bwalo la chakula na kupeleka sehemu nyingine k.v. bwenini, darasani au sehemu nyingine yoyote. Kuhusu wagonjwa matroni na wengine wanaohusika watahakikisha kuwa wamepelekewa chakula stahiki (**ufafanuzi wa Sheria za Shule no. 20**).

4) Ifahamike kuwa mwanafunzi akichelewa kwenda mezani, chakula chake kitagawanywa kwa wenzake. Kanuni hii ni kwa ajili ya kumsaidia mwanafunzi kuwa kwenye sehemu ya tukio kwa wakati uliopangwa (**ufafanuzi wa Sheria za Shule no. 05**).

5) Mavazi yote ya binafsi wanayovaa wanafunzi nje ya sare zao za shule, lazima yawe ya heshima. Kwa wasichana hairuhusiwi kuvaa suruali au kaptula za aina yoyote, tops aina zote, na nguo nyingine zisizo za heshima. Kwa wavulana hawaruhusiwi kuvalia suruali kwenye makalio na kuacha vishikizo

vya mashati bila kufunga. Hakuna haja ya kuleta nguo nyingi hapa shuleni. Mwanafunzi yupo hapa kwa muda maalumu na kwa ajili ya kusoma na kupata malezi tu, si mahali pa kuvaa nguo za mitindo na kuoneshana utajiri wa nguo.

6) Siku ya kufungua shule kutakuwa na ukaguzi kwa watoto wenu. Baada ya mwanao kukaguliwa na kuruhusiwa kujiunga na shule yetu, unatakiwa kuagana naye sehemu ya ukaguzi na kumwacha mikononi mwa uongozi wa shule **bila kuingia bwenini kwake**, vinginevyo mzazi/mlezi utadaiwa kuwa umempatia mwanao vitu (simu za mkononi, line ya simu, pesa, n.k.) kwa kificho na hivyo kuvuruga kanuni za ukaguzi wa shule. **Kosa hilo litakufanya urudi na mwanao nyumbani ili ukamtafutie shule nyingine.** Ifahamike wazi kuwa mwanafunzi atakayechelewa kufika shuleni tarehe iliyopangwa kufungua shule, **hatapokelewa shuleni (ufafanuzi wa Sheria za Shule no. 14)**.

7) Ikiwa wazazi/walezi hawaishi hapa Dar Es Salaam, wazazi/walezi wamtaje ndugu au rafiki atakayesimama kwa niaba ya wazazi/walezi wa mtoto. Mwakilishi huyu pia atachukua madaraka yote ikiwa itatokea shida na hasa wakati mtoto anaumwa.

8) Kadiri inavyowezekana matibabu ya meno au macho (miwani) yafanyike wakati wa likizo. Mwanafunzi akiumwa shuleni k.m. kichwa, tumbo na vitu vingine vya kawaida atamwona mwangalizi wa bweni (Matroni) anayetoa huduma ya kwanza kwa muda uliopangwa. Kama kutakuwa na tatizo zaidi wazazi/walezi atataarifiwa ili amchukue na kumpeleka hospitali kwa matibabu zaidi.

9) Uongozi wa shule unasisitiza kuwa: mwanafunzi haruhusiwi kukaa na dawa za aina yoyote bwenini au mahali pengine. Dawa zote zitakaa kwenye ofisi ya Matroni. Wanafunzi, wazazi/walezi hawaruhusiwi kupeana dawa bila idhini ya uongozi wa shule. Ikumbukwe kuwa hata kama mzazi/mlezi ni daktari wa binadamu hatatoa dawa kwa mwanafunzi hapa shuleni kinyemela bila idhini ya uongozi wa shule.

10) Wanafunzi wote lazima wahudhurie vipindi vyote kama Ratiba ya Shule inavyoonesha. Kazi za mikono (usafi wa mazingira, mabweni, n.k) ni sehemu ya elimu na malezi yanayotolewa hapa shuleni. Kwa hiyo kila mwanafunzi atashiriki kikamilifu bila kutoa visingizio (**angalia Sheria za Shule no. 02 na 03**).

11) Hakuna ruhusa kwa mwanafunzi kuongea na mgeni yeyote, au mfanyakazi asiyehusika naye. Wageni wa kupita hawaruhusiwi kuongea na wanafunzi, ila tu ikiwa ni mmoja wa wazazi/walezi ambao watafika kuongea nao siku maalumu ya kuwatembelea wanafunzi. Vijana/watoto hawaruhusiwi kutumwa shuleni kuleta vitu mbalimbali au kuongea na mwanafunzi. Siku ya kuwatembelea wanafunzi ni kuanzia saa 8:00 mchana hadi saa 11: 30. Wazazi/walezi wataongea na wanafunzi ndani ya eneo la shule tu, ni marufuku kabisa kutoka na wanafunzi nje ya eneo la shule (**angalia Sheria za Shule no. 07 na 08**).

12) Barua zote ziendazo nje ya eneo la Shule hazina budi zipitie kwa mtu anayehusika na si kuzipeleka kwa njia nyingine. Jambo la kupeleka na kupokea barua kinyemela na kununuliwa vitu kinyemela vitamsababishia mwanafunzi kukatishwa masomo na kurudishwa nyumbani kwa muda (suspension).

13) Ni marufuku kuandika au kuchora kwenye vitabu vya shule, ukutani, madawati au ubao (Blackboard na whiteboards). Mwanafunzi aliyebainika kuandika kitabu/vitabu, kitabu/vitabu hivyo havitapokelewa na badala yake mzazi/mlezi atalazimika kununua au kulipa gharama ya kitabu/vitabu husika (**angalia Sheria za Shule no. 12**).

14) Wakati wa likizo hakuna mwanafunzi atakayeruhusiwa kubaki Shuleni kwa sababu yo yote ile. Kwa hiyo ni jukumu la mzazi/mlezi kuhakikisha mtoto wake analetewa nauli mapema iwezekanavyo ili kuepukana na tatizo hilo. Nauli italetwa hapa shuleni kwa mhasibu wa shule si mahali pengine. Mtoto atakayechelewa hapa shuleni, mzazi atalipa kila siku **Tshs 30,000/** kama sehemu ya hosteli ya mtoto wake kukaa hapa nje ya muda wa shule.

……..……	……..……	……..……
Fr. Erastus Mgani, OSA	**Fr. Urick Kinyero, OSA**	**Fr. Gontardo Matavika, OSA**
Mkuu wa Shule	**Mwalimu wa Taaluma**	**Mwalimu wa Nidhamu**